

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO  
TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO  
(TaSUBa)



## FURSA YA UFADHILI WA MASOMO YA SANAA “SANA TUITION FEE WAIVER SCHOLARSHIP” KWA MWAKA WA MASOMO 2018/2019

### 1. UTANGULIZI

Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo – TaSUBa (Zamani Chuo cha Sanaa Bagamoyo) ni wakala wa Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambayo inatoa mafunzo, inafanya utafiti na kutoa ushauri katika sanaa na utamaduni. Malengo ya TaSUBa ni kuendeleza na kukuza sanaa na utamaduni kwenye nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutoa mafunzo, ushauri, kufanya utafiti na kuendesha matamasha, warsha na makongamano. Mnamo mwaka 2012 TaSUBa ilitangazwa kuwa Kituo chenye Uhora Uliotukuka cha Maendeleo ya Sanaa na Utamaduni Afrika Mashariki.

TaSUBa inapenda kutangaza fursa ya ufadhili wa masomo ya Sanaa “Sanaa Tuition Fee Waiver Scholarship” kwa mwaka wa masomo 2018/2019. Ufadhili huu utahusu Ada ya masomo tu, gharama nyingine (Chakula, Malazi, Vifaa vya kuandikia, Matibabu na Usafiri) zitagharamiwa na wanafunzi wenyewe. Ufadhili umeanzishwa kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi wa kike wa wakitanzania, wenye vipaji katika sanaa ili waweze kuendeleza vipaji vyao. Jumla ya wanafunzi watakaofadhiliwa ni 12 kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kiwango cha Kozi: Ufadhili unatolewa kwa waombaji wa **Astahada ya mwaka mmoja** katika kozi zifuatazo:

- i. Astahada ya Sanaa za Maonyesho na Ufundi
- ii. Astahada ya Uzalishaji wa Picha Jongevu
- iii. Astahada ya Uzalishaji wa Muziki na Sauti.

## **2. VIGezo VYA KUJIUNGA**

- a) Mwombaji anatakiwa kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- b) Mwombaji anatakiwa kuwa na afya njema.
- c) Mwombaji anatakiwa awe na elimu ya Kidato cha Nne mwenye ufaulu wa angalau masomo manne (4).
- d) Mwombaji anatakiwa kuwa na umri usiozidi miaka 25.

## **3. JINSI YA KUOMBA**

3.1 Fomu ya maombi ya ufadhili wa masomo ya Sanaa “Sanaa Tuition Fee Waiver Scholarship” inapatikana kwenye tovuti ya chuo [www.tasuba.ac.tz](http://www.tasuba.ac.tz).

3.2 Maombi yaambatanishwe na:

- i. Nakala ya Fomu ya Maombi iliyojazwa vizuri.
- ii. Nakala ya Cheti cha kumaliza Elimu ya Kidato cha Nne.
- iii. Barua ya mapendekezo kutoka BASATA au Ofisi za Utamaduni katika Halmashauri za Wilaya, Mkoa, Mji, Jiji au Manispaa.
- iv. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

3.3 Maombi yatumwe kupitia barua pepe [tasuba@habari.go.tz](mailto:tasuba@habari.go.tz) ikiwa na kichwa cha habari “Sanaa Tuition Fee Waiver Scholarship – 2018/2019”.Mwisho wa kuomba ufadhili wa masomo ni tarehe 15 Agosti 2018.

## **ANGALIZO:**

1. Ufadhili wa masomo unahusu Ada, Fedha ya tahadhari, Ada ya Umoja wa Wanafunzi, Ada ya uthibiti ubora na Kitambulisho .
2. Mwombaji anatakiwa kujigharamia chakula, malazi, usafiri, vifaa vya kuandikia (Stationaries), na gharama za matibabu. Kwa mchanganuo wa gharama hizi,tafadhali tembelea [www.tasuba.ac.tz](http://www.tasuba.ac.tz)
3. Watakaomba kwa kutumia “Testimonial”, “Provisional Results”, “Statement of Results” maombi yao HAYATAKUBALIWA.
4. Maombi ambayo hayatakuwa na viambatisho husika hayatafikiriwa katika Ufadhili.
5. Waombaji watakaopata fursa ya ufadhili wa masomo watajulishwa kuanzia tarehe 14 Septemba 2018.
6. Waombaji ambao ni waajiriwa wa Serikali ni lazima wapate ruhusa kutoka kwa waajiri wao.

Imetolewa na:

Mtendaji Mkuu,

Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)

S.L.P 32, BAGAMOYO.

Barua pepe: [tasuba@habari.go.tz](mailto:tasuba@habari.go.tz) Simu: +255 (0)23 2440032, 0763408792, 0655840405, 0713297626 au 0683993401

Tovuti: [www.tasuba.ac.tz](http://www.tasuba.ac.tz)